



Ili Kupambana na kuenea kwa COVID-19 ndani ya Michigan, Gavana Whitmer alisaini Agizo la Mtendaji 2020-71 ili kuweka hatua za usalama kulinda umma na wafanyakazi kutokana na kukabiliwa na COVID-19. Ni muhimu na busara kuweka viwango kwa uuzaji wa chakula (pamoja na, lakini sio mdogo na, maduka ya mboga, maduka ya vitu vidogo, mikahawa inayouza mboga au chakula inayopatikana kwa kuchukua) na maduka ya dawa ili kupunguza hatari ya kuathiriwa na COVID-19 na maambukizi ya magonjwa. Vitu muhimu vya agizo hili la mtendaji vimeorodheshwa hapo chini. Agizo hilo linafaa kutekelezwa mara moja na kuendelea hadi Mei 30, 2020. Unaweza kukagua agizo lote wavuti ya serikali hapa [on safety measures to protect consumers and employees on the state's website.](#)

### **Kwa Ulinzi wa Mtumiaji na Mfanyikazi**

- Mtu yeyote anayeingia kwenye uuzaji wa maduka ya chakula au maduka ya madawa ambaye kimatibabu huweza kuvumilia vifuniko vya uso lazima avae kifuniko juu ya pua na mdomo wake, kama vile maski iliyotengenezewa nyumbani, kitambaa, bandana au lesa
- Vituo vya kuuza chakula na maduka ya madawa lazima waunde angalau masaa 2 kwa wiki ya wakati wa ununuzi uliowekwa kwa idadi ya watu walio katika hatari ya kuathiriwa ikiwa ni pamoja na watu walio na umri zaidi ya miaka 60, wajawazito na wale walio na hali sungu ya kiafya.
- Vituo vya kuuza chakula na maduka ya dawa lazima wahakikishe kuwa wako na vifaa vya kunawia mikono.
- Wafanyakazi wanaohudumia moja kwa moja wateja wanalazimika kuvaa maski iliyotengenezewa nyumbani, barali, bandana au lesa
- Vituo vya kuuza chakula na maduka ya madawa lazima zihakikishe wafanyakazi na wateja hubakia kwa umbali angalau mita sita kwa kiwango cha juu iwezekanavyo (pamoja na wakati wa mapumziko ya wafanyakazi).
- Vituo vya chakula vilivyotayarishwa kama vile baa za saladi lazima zifungwe, na sampuli za bure na vituo vya kuonja lazima viondolewe.
- Vituo vya kuuza chakula na maduka ya madawa lazima vitekeleze taratibu za kukidhi miongozo ya kusafisha mazingira iliyowekwa na CDC, pamoja na kusafisha vifaa vinavyoguswa mara kwa mara kama vile sehemu ya vituo vya kuuza kwenye kuoredhesha, vigari vya ununuzi, na vikapu vya ununuzi.
- Vituo vya kuuza chakula na maduka ya dawa lazima wapige marufuku wafanyakazi ambao ni wagonjwa kuripoti kazini na lazima watume wafanyakazi nyumbani ikiwa wataonyesha dalili za COVID-19.
- Ikiwa mfanyakazi katika kituo cha uuzaji wa chakula ataambukizwa COVID-19, kituo hicho kitahitajika kuwaarifu wachuuzi wa chakula na wafanyakazi wengine haraka iwezekanavyo lakini sio kabla ya masaa 12 baada ya kupokea uthibitisho wa maambukizi hayo bila kufichua hali ya kiafya ya kibinafsi ya mfanyakazi yeyote.
- Vituo vya kuuza chakula na maduka ya amadawa lazima vizingatie wafanyakazi ambao huangukia katika idadi ya watu walio hatarini kwa kuwapa kazi zilizo katika hali ndogo ya maambukizi au kuwapa chaguo la kuchukua likizo isiyo na malipo na uthibitisha wa tarehe ya kurudi kazini pamoja na matokeo ya mwisho ya kutangaza hali ya dharura na janga katika jimbo, au Mei 21, 2020 (tarehe yoyote ambao itakuwa ya nyuma).
- Vituo vya kuuza chakula na maduka ya dawa vinahitajika kukuza na kutekeleza mpango wa uchunguzi wa kila siku kwa//// wote kabla ya kuripoti kwenye vituo vya kazi. Maelezo ya mpango wa uchunguzi yanapatikana katika [are included in the executive order.](#)

Habari ya hivi karibuni ya COVID-19 inapatikana katika [Michigan.gov/Coronavirus and CDC.gov/Coronavirus.](#) Kwa wale ambao wana maswali kuhusu hatua za serikali za kupunguza kuenea kwa virusi vya corona, tafadhali ita COVID-19 1-888-535-6136 kati ya saa 8 asubuhi na saa 5 jioni kila siku.